

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



BUNGE LA TANZANIA

MWONGOZO WA SPIKA

KUHUSU

**UTARATIBU WA KURATIBU WAGENI
WANAOTEMBELEA MAENEO YA BUNGE**

MWONGOZO WA SPIKA

Waheshimiwa Wabunge, asubuhi ya leo Mhe. Kasuku Samson Bilago(Mb)aliomba mwongozo wangu kuhusu utaratibu unaotumiwa na askari wa Bunge kuwataka wageni wanaokuja kutembelea kuacha vitambulisho na simu zao getini wakati wanapoingia katika maeneoya Bunge. Baada ya kuombwa mwongozo huo niliomba nipatiwe muda kidogo ilinifanyie kazi jambo hilo.

Waheshimiwa Wabunge, utaratibu wa wageni kutembelea maeneoya Bunge ikiwa ni pamoja na humu ndani ya ukumbi wa Bunge umewekwa kwa mujibu Kanuni za kudumu za Bunge, sehemu ya Kumi na Saba inayohusu usalama wa maeneo ya Bunge. Sehemu hii ya Kanuni kupitia Kanuni ya 144 na 145 imeweka utaratibu wa kuingia katika maeneo ya Bunge na utaratibu wa ukaguzi kwa mtu yeyote anayeingia katika maeneo ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge,Aidha kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi ya kuratibu wageni wanaotembelea Bunge na maeneo mengine ya Bunge, Mpambe wa Bunge chini ya Kanuni ya 20(1) inayomtaka kusimamia masuala yote ya ulinzi na usalama wa ofisi, mali, vifaa na majengo yote ya Bunge baada ya kushauriana na uongozi wa Bunge aliamua kuweka utaratibu ambao umeanza kutumika muda mrefu kwa kuwataka watu wote wanao kuja kutembelea maeneo ya Bunge kuacha vitambulisho vyao(kama vile kitambulisho cha kazi, leseni ya udereva, kitambulisho cha mpiga kura au kitambulisho cha bima

ya afya) au kama hawana moja ya vitambulisho tajwa hapo juu basi wa natakiwa kuacha simu zao getini kwa ajiliya utambuzi na dhamana ya kuhakikisha wanarejesha vitambulisho wanavyopatiwa wakati wakiingia katika maeneo ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, huo ni utaratibu wa kawaida kabisa ambao hutumika hata katika ofisi nyingine za binafsi na za umma, hivyo naomba kwa pamoja tushirikiane kuwaelimisha wananchi ambao ni wapiga kura wetu kuhusu utaratibu huo ili waweze kuzingatia na kutoa ushirikiano unaohitajika katika kulinda usalama wetu na wa maeneo ya Bunge kwa ujumla.

Waheshimiwa Wabunge, kimsingi utaratibu huo na mashartiya Kanuni tajwa hapo juu yanalenga kulinda na kuhakikisha usalama wetu sisi Wabunge na maeneo ya Bunge kwa ujumla wake.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndio mwongozo wangu kuhusu utaratibu kwa wageni wanaotembelea maeneo ya Bunge.

Umetolewa leo tarehe 17 Mei, 2016

Job Y. Ndugai (MB)

SPIKA